## Kuunga Mkono kwa Uteuzi wa Siku ya Kitaifa ya Uhamasishaji wa VVU/UKIMWI na Homa ya ini (Hepatitis) kwa Mhamiaji na Mkimbizi wa Kiafrika- Septemba 9

Sisi mashirika yaliyotia saini, sote tumejitolea kupunguza tofauti za kiafya zinazohusiana na VVU/UKIMWI na homa ya ini aina ya B (Hepatitis B) miongoni mwa jamii zilizoathiriwa sana kwa kuongeza uhamasishaji, uchunguzi, kinga, na kuwaunganisha na huduma za utunzaji, tunatoa wito wa kuteuliwa rasmi kwa siku ya kitaifa ya uhamasishaji wa VVU/ UKIMWI na homa ya ini (Hepatitis) kwa mhamiaji na mkimbizi wa kiafrika (NAIRHHA), inayoadhimishwa kila mwaka tarehe 9 Septemba , kama maadhimisho ya kitaifa ya afya.

Idadi ya wahamiaji na wakimbizi wa Kiafrika wanaoishi Marekani iliongezeka kwa 500% kati ya 1980 na 2016, na jamii hizi zinatarajiwa kuendelea kukua kwa kiwango cha juu - takwimu ya sensa ya Marekani imeonyesha kuwa idadi ya wahamiaji wa kiafrika iliongezeka kwa 71% kati ya mwaka wa 2001- 2016. Viwango vya maambukizi ya VVU ni mara sita zaidi katika idadi ya wahamiaji wa kiafrika kuliko idadi ya jumla ya watu Marekani. Wahamiaji wa kiafrika pia wanakabiliwa na wastani wa juu zaidi ya viwango vya virusi sugu vya homa ya ini aina ya B (Hepatitis B) nchini, na takriban 10% ya jamii hizi wanaishi na homa ya ini (Hepatitis B). Kutokana na kuenea kwa homa ya ini aina ya B (Hepatitis B) katika maeneo mengi barani Afrika, kituo cha udhibiti wa magonjwa (CDC) inapendekeza kuwa watu waliozaliwa Afrika au watu waliozaliwa Marekani ambao wana angalau mzazi mmoja aliyezaliwa Afrika, ambao hawakuchanjwa wakati wa kuzaliwa, wanapaswa kupewa kipaumbele kwa kupima homa ya ini ania ya B (Hepatitis B).

Jamii za wahamiaji wa kiafrika zinakabiliwa na changamoto kubwa kwa upimaji wa VVU na virusi vya homa ya ini (Hepatitis), matunzo, pamoja na matibabu: Ingawa wana viwango vya juu vya maambukizi, jamii hizi zina viwango vya chini vya utambuzi na utunzaji. Changamoto ni pamoja na unyanyapaa, woga, ukosefu wa ufahamu na ujuzi, vikwazo vya lugha, maadili ya jadi na kanuni za kijamii, na ugumu wa kupata huduma za afya. Hali ya uhamiaji pia inahusishwa na woga wa vituo vya afya, kutobadili tamaduni na kutokufahamu kuzunguka mifumo tata ya huduma za afya, kutengwa kijamii na kiuchumi, woga wa kufukuzwa nchini, na kiwango cha chini cha bima ya afya, yote yakiwa ni vikwazo vikubwa kwa afya ya wahamiaji na wakimbizi wa kiafrika wanaoishi Marekani. Pia kuna haja ya huduma na watoa huduma kufaa kitamaduni na kuwa sahihi kiisimu ili kukidhi vyema mahitaji ya wahamiaji wa kiafrika, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa vya huduma zinazofaa kitamaduni na sahihi kiisimu (CLAS) katika afya na huduma ya afya, ambayo inaelelzea mfumo wa kutoa huduma ambazo ni za heshima na nyeti kwa lugha na utamaduni, na zinazojibu utamaduni wa afya ya mgonjwa, imani, mapendeleo, na mahitaji ya mawasiliano.

VVU na homa ya ini aina ya B na C (Hepatitis B and C) ni hali zinazoweza kuzuilika na zinazoweza kutibika - kwa umakini na kuzingatia ipasavyo, matokeo ya afya miongoni mwa jamii za wahamiaji za kiafrika yanaweza kuboreshwa na maisha yanaweza kuokolewa. Siku ya NAIRHHA ni siku inayolenga kuleta umakini wa eneo na kitaifa kwa masuala ya afya ya VVU/UKIMWI na virusi vya homa ya ini (Hepatitis) kwa wahamiaji na wakimbizi wa kiafrika nchini Marekani, kwa njia ambayo inafaa kitamaduni na kiisimu. Kwa kushughulikia baadhi ya masuala ya kipekee ambayo wahamiaji wa kiafrika nchini Marekani wanakabiliana nayo kupitia uhamasishaji, elimu, na rasilimali, siku ya NAIRHHA itasaidia kuziwezesha jamii kutunza afya zao wenyewe.

Malengo ya siku ya NAIRHHA ni pamoja na: (1) kuongeza uelewa na kuondoa unyanyapaa; (2) elimu kuhusu njia za kinga na matibabu ya VVU, virusi vya homa ya ini (Hepatitis) na magonjwa mengine yanayohusiana; (3) kurejesha udhibiti ndani ya jamii kwa kuhimiza uchunguzi na matibabu, pamoja na chanjo ya homa ya ini aina ya B (Hepatitis B); na (4) kutetea sera na desturi zinazokuza afya ya jamii,familia na ata watu binafsi miongoni mwa wahamiaji wa kiafrika . Kwa sasa hakuna siku ya uhamasishaji kuhusu VVU/UKIMWI ambayo inashughulikia mambo tofauti yanayoathiri viwango vya juu vya VVU na virusi vya homa ya ini (Hepatitits) kwa wahamiaji na wakimbizi wa kiafrika. Vikundi hivi mara nyingi hupuuzwa au kuainishwa vibaya kama "Mweusi" au "mmarekani mwenye asili ya kiafrika" katika programu za ufuatiliaji wa VVU, kwa sababu ya mifumo ya upelelezi kutokusanya au kuripoti data kuhusu nchi ya asili.

Kutokana na ongezeko la haraka la idadi ya wahamiaji wa kiafrika nchini Marekani, ni muhimu kuongeza uelewa miongoni mwa jamii hizi, na watoa huduma za afya, na watoa huduma za kijamii wanaowahudumia na kuhusu hatari ya ugonjwa wa homa ya ini (Hepatitis) na VVU/UKIMWI, matokeo yanayoweza kuwa , na fursa za kuzuia, uchunguzi na matibabu. Wahamiaji wa kiafrika wanapokuwa wakaaji wa muda mrefu wa Marekani, itakuwa muhimu zaidi kutoa huduma za uchunguzi, kuzuia, na matibabu ya magonjwa sugu na ya kuambukiza kwa kutumia mbinu inayofaa ya kitamaduni na inayofaa kiisimu. Kujenga uwezo ndani ya jamii ili kukuza ujuzi kuhusu matibabu na kuzuia VVU na virusi vya homa ya ini (Hepatitits) huchangia pakubwa katika uendelevu wa mpango wa siku ya NAIRHHA. Kadri jamii zinavyoongeza uwezo wao wa kukabiliana na "majanga kimya'' ya VVU na virusi vya homa ya ini (Hepatitis), watazalisha rasilimali ili kuendeleza kazi hii. Kwa kuhimiza watu wengi zaidi kupima na kupata matibabu, siku ya NAIRHHA inasaidia katika kupunguza maambukizi mapya. Kwa kujaribu kupunguza na hatimaye kuondoa unyanyapaa unaohusiana na VVU/UKIMWI na virusi vya homa ya ini (Hepatitis), siku ya NAIRHHA inawezesha ujenzi wa jamii na mawasiliano.

Kuteuliwa kwa Septemba 9 kama "Siku ya Kitaifa ya Wahamiaji na Wakimbizi ya VVU/UKIMWI na virusi vya homa ya ini (Hepatitis) (NAIRHHA)," kutatambua umuhimu wa kuweka umakini na rasilimali zaidi kushughulikia VVU/UKIMWI na virusi vya homa ya ini (Hepatitis) katika jamii za wahamiaji na wakimbizi wa kiafrika kote Marekani, na ingehimiza dhamira ya kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya homa ya ini (Hepatitis) na VVU na homa ya ini ya B- na C- (Hepatitis B and C) na vifo vinavyohusiana na VVU kupitia uchunguzi thabiti zaidi, chanjo, na kuunganishwa na matibabu na matunzo katika jamii za wahamiaji na wakimbizi wa kiafrika.

Imetiwa saini

Muungano wa tamaduni nyingi za UKIMWI (Multicultural AIDS Coalition)

Shirika la Hepatitis B (Hepatitis B Foundation)